# Dhana ya Uambikaji katika Kiswahili

*Arnold Gawasike*

*Ikisiri*

Lugha ya Kiswahili inaunda msamiati wake kwa kutumia njia mbalimbali ili kukidhi haja ya mawasiliano. Miongoni mwa njia zinazotumika kuunda msamiati huo ni pamoja na uambishaji na unyambulishaji. Katika Kiingereza njia hizi zinaelezwa kwa urahisi na zinaeleweka. Hali ni tofauti katika Kiswahili. Makala haya yanafafanua dhana hizi, na kwa kutumia dhana ya uambikaji inajadili uhusiano uliopo baina yake. Pili, kwa kutumia mifano na maelezo kuntu kutoka katika Kiswahili, makala yanapendekeza dhana ya uambikaji (Affixation) kutumika kama msingi wa kuonesha uhusiano huo ili kuondoa mkanganyiko uliopo.

## 1. 0 Utangulizi

Dhana ya uambikaji katika Kiswahili kwa namna tofauti tofauti imejadiliwa na baadhi ya wanaisimu wa Kiswahili kama vile: Nkwera (1978), TUKI (1990), Rubanza (1996), Kihore na wenzie (2003) na Massamba (2004) kwa kutaja wachache. Katika makala haya tunakusudia kutengua mitazamo iliyozoeleka kuhusu dhana hii na kubainisha kwa mifano baadhi ya mapengo yaliyosalia katika dhana hizi.  Aidha, makala yatapendekeza dhana ya uambikaji itumike badala ya uambishaji kama ilivyotumiwa na wanaisimu wengine waliotangulia kuandikwa. Mifano na mijadala itajikita katika Kiswahili.


## 1.1 Fasili ya Dhana

Massamba (2004) anafasili dhana ya uambishaji (affixation) kuwa ni taaluma ya mofolojia inayohusu utaratibu wa kuweka kiambishi kabla, katikati au baada ya mzizi. Anabainisha kuwa kuna aina mbili za uambishaji: uambishaji nyambulishi (Derivation) na uambishaji kisarufi (inflection). Maelezo haya yanaoana na yale ya TUKI (1990) ambao wanaeleza kwamba uambishaji ni utaratibu wa kuweka kiambishi kabla, katikati au baada ya mzizi. Aidha, Kihore na wenzie (2003) wanaeleza kuwa katika Kiswahili viambishi hujitokeza kabla au baada ya mzizi wa neno. Tunakiri hapa kuwa dhana ya uambikaji ambayo ndiyo tunayoipendekeza kutumika ili kuonesha uhusiano uliopo baina ya unyambulishaji na uambishaji inajitokeza katika andiko la Rubanza (1996). Tazama kielelezo namba 1 hapa chini.

Maelezo ya Massamba (2004) na TUKI (1990) yanayodai kuwa uambishaji ni utaratibu wa kuweka kiambishi kabla, katikati na baada ya mzizi wa neno hayaoneshi uhusiano wa dhana hizi mbili; uambishaji na unyambulishaji. Dhana hizi mbili zinajumuishwa katika dhana ya *Uambikaji*. Kwa maneno mengine dhana za uambishaji na unyambulishaji zimebebwa na dhana hiyo ya

uambikaji. Dhana hizi zinaelezwa katika Kiswahili kana kwamba ni dhana ambazo kila moja inajisimamia yenyewe. Ni kutokana na mazoea haya ndiyo maana waandishi kama Nkwera (1978), TUKI (1990 na 2004) na Kihore na wenzie (2003) wamezichanganya kabisa. Ukisoma kazi hizi wakati mwingine unashindwa kubaini iwapo ipo tofauti ya dhana hizi.

Aidha, ukichunguza maelezo na fasili zote hizi hazielezi chochote kuhusu dhana ya uambikaji. Rubanza (1996) anaona kuwa unyambulishaji ndiyo dhana kuu iliyogawanyika katika sehemu tatu: *Uambikaji, Mzizi na Unyambuaji* ikiwa katika mtindo wa ungoe. Tazama kielelezo Na. 1 hapa chini kwa mfano:




Kielelezo Na. 1: Unyambulishai kama dhana kuu

***Chanzo:*** *Rubanza (1996:90)*

Kutokana na kielelezo hiki, maneno katika mfano ufuatao 1(a)–(d) yanaonesha kuwa yamefanyiwa unyambulishaji.

1. (a) wa-me-m-**tembe**-le-a
   (b) a-li-**pat**-ik-an-a
   (c) tu-ta-wa-**og**-esh-a
   (d) m-na-ni-**safish**-i-a.

Mtazamo wetu hapa ni kuwa dhana ya uambikaji ndiyo itumike badala ya unyambulishaji lakini ikiwa ndiyo dhana kuu au dhana pana kuliko uambishaji na unyambulishaji, kama tulivyokwishakueleza hapo awali.

Aidha, hatuna tatizo na fasili pamoja na mifano iliyotolewa na Rubanza (1996). Kinachosisitizwa hapa ni kwamba kuna haja ya kuelezwa kwa namna nyingine dhana hii. Fasili ya unyambuaji kwa mujibu wa Rubanza (keshatajwa) ni upachikaji wa viambishi vinavyofuata mzizi. Fasili hii inahitaji kuangaliwa kwa namna nyingine kulingana na maana ya msingi ya neno `nyambua’.

Kunyambua ni kuchambua kitu kilichoshikamana au kuvuta na kuongeza urefu wa kitu chenye kuvutika, mfano mpira (TUKI, 2004). Unyambuaji ni utenganishaji wa kitu mathalani mofu zinaweza kutenganishwa kutoka katika mzizi wa neno. Hivyo, kutokana na msingi huo na uelewa wetu wa kimalimwengu, unyambuaji hauhusiani tu na uongezaji wa viambishi baada ya mzizi au urefushaji wa kitu. Unyambuaji unaofasiliwa na Rubanza unarejelea mchakato wa utenganishaji wa mofu katika neno.

Kama tulivyoeleza hapo awali, makala haya yanapendekeza dhana ya Uambikaji kuwa ndiyo dhana kuu ikijumuisha dhana ya uambishaji na unyambulishaji. Wazo hili si wazo jipya kwani linajitokeza katika Anderson (1992) na Aronoff (1994) kwa nyakati tofauti walipodai kuwa dhana ya uambikaji ni mchakato wa kifonolojia unaohusisha viambishi vya neno zima. Msimamo wa makala haya ni kwamba uambikaji ni mchakato wa kimofolojia ambao unahusu uongezaji wa mofu[1] (viambishi) kabla na baada ya mzizi wa neno. Mifano katika 2(a) – (d) hapa chini ina inashadidia hali hiyo.


| | **Neno** | **Ubainisho wa mofu** |
|---|---|---|
| 2. | (a) Anayemsomeshea | a-na-ye-m-**som**-esh-e-a |
| | (b) Waliwapatanishia | wa- li- wa-**patan**-ish-i-a |
| | (c) Tumependelewa | tu-me-**pendele**-w-a |
| | (d) Nitakayembembelezea | ni-taka-ye-m-**bembelez**-e-a |

Mifano hiyo inaonesha kuwa uambikaji unahusu upachikaji wa viambishi (mofu) kabla na baada ya mzizi wa neno. Sehemu ya neno iliyokozwa katika maneno hayo ndiyo mzizi wa neno husika.

## 2.0 Aina za Uambikaji

Kama tulivyodokeza hapo awali, uambikaji ni upachikaji wa mofu kabla na baada ya mzizi wa neno. Aidha, uambikaji ni dhana ya juu ambayo imegawanyika katika sehemu mbili, uambishaji na unyambulishaji. Msingi wa mgawanyo wake ni mzizi wa neno. Tunatumia kielelezo Na. 2 kuonesha aina za uambikaji na uhusiano wake kiutawalia:

[1] Mofu ni umbo halisi linalowakilisha mofimu. Kimsingi kinachopachikwa katika mzizi wa neno sio mofimu kama inavyodaiwa na wanamapokeo na baadhi ya wanaisimu wa sasa. Mofimu ni dhana dhahania iliyopo kichwani au akilini mwa mtumia lugha na sio umbo halisi.




**Kielelezo Na. 2: Aina za Uambikaji na Uhusiano wa kiutawalia**

Kielelezo hiki kinaonesha kuwa uambikaji ni dhana ya juu (kiambajengo cha juu) ikiundwa na viambajengo sisisi ambavyo ni uambishaji na unyambulishaji. Mzizi ndiyo msingi au mpaka wa mgawanyo wetu. Aidha, mwainisho huu unaafikiana na mawazo ya Anderson (1992) na Aronoff (1994) ambapo kwa nyakati tofauti walipata kueleza kuwa uambikaji ni mchakato wa kifonolojia unaohusisha ungoekaji wa viambishi katika neno zima. Hata hivyo, msimamo kuhusu hoja yao hiyo ni kuwa tunakubaliana na dai kuwa uambikaji unahusu ungoekaji wa viambishi kwa neno zima lakini tofauti na wao, dai la makala haya ni kuwa uambikaji ni mchakato wa kimofolojia na sio kifonolojia. Sehemu inayofuata inajadili dhana hizi katika muktadha wa Kiswahili.

## 2. 1 Dhana ya Uambikaji katika Kiswahili

Uambikaji ni njia mojawapo inayotumika katika kuunda maneno katika lugha kwa kuongeza mofu au viambishi katika mzizi wa neno. Uongezaji huu katika muktadha wa Kiswahili hufanyika kabla na au baada ya mzizi wa neno. Aidha, uambikaji unaweza kutoa tungo ambazo ni sentensi sahihi kwa sababu maneno yanayoundwa huonesha mtendaji wa tendo, wakati tendo lilipotendeka, na anayetendewa tendo hilo. Kwa mfano:

| | **Neno** | **Ubainishao wa mofu** |
|---|---|---|
| 3. | (a) analimishwa | a- na- **lim**- ish-w-a |
| | (b) mliyesukana | m- li- ye- **suk**- an-a |
| | (c) watamsomeshea | wa- ta-m-**som**- esh-e- a |

Katika mifano 3 (a), (b) na (c) mofu {a-}, {m-} na {wa}- zinawakilisha mtenda wa jambo katika tungo hizo. Aidha, katika mifano hiyohiyo mofu {-na-}, {-li-}, na {-ta-} zinawakilisha wakati (meo) ambapo tendo hilo lilifanyika. Vilevile maumbo {-suk-}, {-lim-} na {-som-} ni mzizi au kiini cha tungo hizo. Katika mfano wa 3 (c) umbo {-e-} linawakilisha utendea (mahali au sababu). Kwenye mfano wa 3 (a) na (c) mofu {-ish-}, {-esh-} zinawakilisha hali ya utendeshi.

Umbo {-w-} katika mfano wa 3 (a) linawakilisha hali ya utendwa. Aidha, katika mfano wa 3 (b) umbo {-an-} linawakilisha hali ya utendana. Wakati umbo {-a} linawakilisha irabu ishilizi. Kwa kuangalia tungo hizo kama tulivyodokeza hapo juu, tunaona mtenda, wakati na mahali au sababu ya tendo kufanyika.

Uambikaji pia, unaweza kubadili maana au kategoria ya neno moja kwenda jingine. Tuchunguze mifano ifuatayo:

| | **Neno** | **Ubainisho wa mofu** |
|---|---|---|
| 4. | (a) ziba | ki-**zib**-o |
| | (b) soma | m-**som**-i |
| | (c) vua | m-**vu**-vi |
| | (d) lima | m-ku-**lim**-a |

Mifano hii katika 4 (a-d) inaonesha kuwa maneno yaliyopo katika safu wima A ni vitenzi, baada ya kuambikwa mofu kabla na baada ya mzizi wa neno, maneno katika safu wima B yamebadili kategoria na kuwa nomino. Uambikaji pia katika Kiswahili na pengine katika lugha nyingine za Kibantu unayo dhima ya kubadili kategoria ya neno, kutoka kategoria moja kwenda nyingine. Mifano katika 4 inadhihirisha dai hilo. Sehemu inayofuata inajadili kuhusu uambishaji.

### 3.0 Dhana ya Uambishaji katika Kiswahili

Uambishaji ni mchakato mojawapo unaotumika katika kuunda maneno katika lugha. Nkwera (1978) ametoa maelezo marefu kuhusu dhana hii akianza na etimolojia ya neno lenyewe kuwa uambishaji linatokana na neno *kuambisha*. Na neno *kuambisha* linatokana na neno *amba* lenye maana (mojawapo) ya kufungia kitu fulani kwenye kitu kingine kipate kubaki pale. Anaendelea kufafanua zaidi kuwa katika Kiswahili kuambisha ni kufungulia au kuongeza mofu fulanifulani mwanzoni au mwishoni mwa mzizi/kiini au shina la neno lolote linalokubali ili kulipa neno hilo hali, tabia na maana mpya au ya ziada, na kuliwezesha neno moja lichukue nafasi mpya katika vishazi. Shughuli nzima ya kufungulia mofu mwanzoni au mwishoni mwa mashina au mizizi ya maneno ndio uambishaji.

Maelezo haya yanatofautiana na yale yaliyowahi kutolewa na TUKI (1990), Rubanza (1996), Kihore na wenzie (2003), Massamba (2004), Nyangwine na Masebo (2007), Khamisi (2009) na Kihore (2009). Kwa mfano, wakati Rubanza (1996) anadai kuwa upachikaji wa mofu (mofimu kama yeye anavyoita) kabla na baada ya mzizi wa neno ni unyambulishaji, Nkwera (1978) anadai kuwa ni uambishaji. Aidha, Nyangwine na Masebo (2007), Massamba (2004) na TUKI (1990) wanauona uambishaji kuwa ni uongezaji wa mofu

(mofimu kama wao walivyoita) kabla ya mzizi wa neno ili kuleta upatanisho wa kisarufi. Madai ya makala haya ni kuwa uambishaji ni uongezaji wa mofu (viambishi) kabla ya mzizi wa neno. Mifano mitano hapa chini inadhihirisha madai haya.

| 5. **Neno** | **Ubainisho wa mofu** |
|---|---|
| (a) hawatatuona | ha-wa-ta-tu-**on-**a |
| (b) tutawatazama | tu-ta-wa-**tazam-**a |
| (c) wametupiga | wa-me-tu-**pig-**a |
| (d) niliyemnunua | ni-li-ye-m-**nunu-**a |

Uambishaji una umuhimu wa kisarufi kama vile kuleta upatanisho wa kisarufi, kuonesha wakati, idadi na kadhalika (Anderson, 1982). Kwa hiyo, fasili inayotolewa na Nkwera (1978) ya uambishaji kwa mujibu wa makala haya inachukuliwa kuwa ni fasili ya uambikaji na sio uambishaji.

Aidha, Kihore na wenzie (2003) wanaeleza dhana hizi (uambishaji na unyambulishaji) bila kuonesha tofauti. Katika sehemu hii tunadurusu suala la uambishaji. Wakinukuu Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (1990) kama msingi wao wa kujenga hoja wanaeleza kuwa uambishaji ni utaratibu wa kuweka kiambishi kabla, katikati au baada ya mzizi wa neno. Kama tulivyoeleza katika 3.2 hapo juu, huo ni uambikaji na sio uambishaji. Wanasisitiza kuwa jambo la muhimu ni kuzingatia mpangilio wa kiambishi au viambishi kutokea kabla na baada ya mzizi. Kwa hakika, maelezo haya yanaleta shida kidogo kueleweka, kwani ni vigumu kubaini tofauti baina ya uambishaji na unyambulishaji. Kwa mfano, tukitumia baadhi ya mifano kama ilivyobainishwa na wataalamu hao (ukurasa 76) kama inavyoonekana katika 6 (a-c) hapa chini inaonekana kuwa uambishaji unaweza kutokea kabla ya mzizi wa neno pekee jambo ambalo tunaafikiana nalo mifano katika 6 (a-c) hapa chini inavyodhihirisha hali hii:

6. (a) ha-wa-ta-tu-**on-**a
   (b) wa-li-o-tu-**tafut-**a
   (c) tu-ta-wa-**tazam-**a

Aidha, hatuna tatizo na mifano hii kwa kuitumia kurejelea dhana ya uambishaji kama ilivyonukuliwa katika Kihore na wenzie (2003). Huu pia ndiyo mtazamo na msimamo wa makala haya kuwa uambishaji unahusu upachikaji wa mofu kabla ya mzizi wa neno. Msisitizo upo katika mtazamo kwamba kile kinachopachikwa katika mzizi wa neno ni mofu na sio mofimu kama Kihore na wenzie (2003) wanavyoeleza.

Pia, uambishaji unachukuliwa na Kihore na wenzie kuwa ni upachikaji wa viambishi kabla na baada ya mzizi wa neno. Wanaisimu hawa inaelekea hawazingatii utenganishaji wa viambishi ikiwa ni sahihi ama la, hasa 7 (f).

7. (d) wa-me-tu-**pig**-an-ish-a
(e) u-li-wa-**nunu**-li-a
(f) *wa-lo-tu-**pend**-ek-ez-a

Mifano hii ina matatizo kidogo kuhusu dhana ya uambishaji. Swali la kujiuliza hapa ni: Je, uambishaji ni nini? Uambishaji na Unyambulishaji ni kitu kimoja? Ikiwa ni kitu kimoja kwa nini kuwe na dhana mbili kuelezea au kurejelea kitu kilekile? Kwa maoni ya makala haya, dhana hizi hazina budi kufasiliwa kwa namna nyingine kidogo. Kama ilivyokwishakuelezwa hapo juu, uambishaji unapaswa kurejelea mifano ya 6 (a-c) pekee, kama ilivyooneshwa na mifano katika 7 (d-f) ambayo inarejelea uambikaji kama tunavyoupendekeza katika makala haya.

## 4.0 Unyambulishaji katika Kiswahili

Dhana ya unyambulishaji kadhalika bado ina uvulivuli kwa baadhi ya wanataaluma katika Kiswahili. Nkwera (1978) kwa mfano anaeleza kuwa mnyambuliko ni ule uwezo wa kufungiliwa mofu (mofimu kama anavyoita) mahususi mwanzoni au mwishoni mwa mzizi au shina la neno. Fasili hii haioneshi tofauti baina ya uambishaji na unyambulishaji. Maoni ya makala haya ni kuwa katika Kiswahili na lugha za Kibantu kwa ujumla Unyambulishaji ni uongezaji wa mofu au viambishi baada ya mzizi wa neno. Uongezaji wa mofu hizi baada ya mzizi wa neno huzalisha kauli mbalimbali hasa kwenye vitenzi. Inasisitizwa katika makala haya kuwa unyambulishaji ni mchakato wa kimofolojia wa uundaji wa maneno kwa kuongeza mofu baada ya mzizi wa neno ili kuzalisha kauli. Aidha, unyambulishaji hujitokeza zaidi na kwa uwazi katika vitenzi. Mifano katika 8 (a-d) inadhihirisha madai haya:

| 8. | **Neno** | **Ubainisho wa mofu nyambulishi** |
|---|---|---|
| (a) | bebeshana | **beb**-esh-an-a |
| (b) | pokezana | **poke**-z-an-a |
| (c) | fagiliwa | **fagi**-li-w-a |
| (d) | somesheana | **som**-esh-e-an-a |

Katika mifano hii, mifano ya 8 (a) na (b) mofu ya utendeshi {-esh-}, {z-} na utendana {-an-} imeongezwa katika mzizi wa neno. Katika mfano wa 8 (c) umbo la utendea {-li-} na umbo la utendwa {-w-} yameongezwa na kwa mfano wa 8 (d) mofu ya utendeshi {-esh-}, utendea }{-e-} na mofu ya utendana {-an} zimeongezwa. Kwa hiyo, mifano yote minne imekamilishwa na irabu ishilizi {-a}.

Aidha, Kihore na wenzie (2003) wanaeleza kuwa unyambulishaji ni uundaji wa maneno unaohusu upachikaji viambishi kabla na baada ya mzizi wa neno. Maelezo haya yanaonesha kuwa wao wanachukulia kuwa uambishaji na unyambulishaji ni kitu kimoja, jambo ambalo makala haya yanaona kuna haja ya kuliangalia upya kama ilivyofanywa katika mifano ya 8 (a-d). Vilevile, Nyangwine na Masebo (2007) wanafasili dhana ya unyambulishaji kuwa inahusu upachikaji wa mofu (mofimu kama wanavyoita) katika mzizi wa neno. Katika mfano unaotokana na mzizi {-lim-}, wanasema tunaweza kupachika mofu (mofimu kama wanavyoita) mbalimbali na kupata maumbo tofauti ya mzizi huo:

9. (a) a-na-lim-a
   (b) m-ku-lim-a
   (c) wa-na-lim-an-a
   (d) *wa-na-limi-an-a

***Chanzo:*** *Nyangwine na Masebo (2007:267)*

Ingawa utenganishaji wa mofu katika 9 (d) unatia shaka ikiwa ni sawa ama la inatosha kueleza kuwa wataalamu hawa nao wanaona kuwa unyambulishaji ndiyo dhana kuu na inatawala uambishaji na mnyambuliko. Kimtazamo hawajaachana na watangulizi wao. Kama tulivyokwisha kueleza hapo juu, kuwa kuchukulia kuwa unyambulishaji ndiyo neno kuu tunadhani pengine mtazamo huu unaweza kutazamwa kwa namna nyingine kama tulivyokwisha kueleza. Maoni ya makala haya ni kuwa kama tulivyoeleza hapo juu, unyambulishaji ni mchakato wa upachikaji mofu baada ya mzizi wa neno ambapo huonesha matokeo ya tendo (tz. 10d) na kuzalisha kauli mbalimbali (taz. 10a-c). Mifano katika 10 inadhihirisha hali hiyo:

10. ( a) **som**-*e*-*an*-a
    ( b) **pig**-*il*-*iw*-a
    (c) **pendez**-*esh*-*w*-a
    (d) **som**-o

Mifano hii inadhihirisha kuwa unyambulishaji unahusika na uongezaji wa mofu (viambishi) baada ya mzizi wa neno. Sehemu ya neno iliyoandikwa hati nzito ndiyo mzizi wa neno na zile mofu ambazo zimeandikwa kwa hati mlalo upande wa kulia mwa mzizi ni mofu mnyambuo, zikifuatiwa kabisa na irabu ishilizi (-a) katika 10 (a-c). Aidha, mofu hizi pia zinaweza kubadili kategoria katika mfano wa 10 (d) ambapo kitenzi `soma' baada ya kupachikwa mofu {-o-}, kimebadilika na kuwa nomino. Pia, mofu zinaweza kutobadili kategoria ya neno bali kuzalisha kauli mbalimbali katika lugha ya Kiswahili; mifano 10 (a-c) inadhihirisha hali hiyo.

**5.0 Hitimisho**

Makala haya yalikusudia kufafanua dhana ya uambikaji katika Kiswahili, ili kuondoa mkanganyiko ambao umekuwapo kwa miongo kadhaa katika sarufi. Katika kufafanua hilo makala yalilenga kupendekeza matumizi ya uambikaji ili kutanzua utata ambao umekuwepo katika dhana za uambishaji na unyambulishaji. Katika kukabili hilo kwa kutumia mifano, imeeleza kuwa uambikaji ni mchakato wa kupachika mofu kabla, katikati na baada ya mzizi wa neno. Katika kufanya hivyo, mchakato huu unaweza kupanua maana ya neno au kubadili kategoria ya neno. Aidha, makala yameeleza kuwa uambishaji ni mchakato wa kupachika mofu kabla ya mzizi wa neno. Umuhimu wa uambishaji ni kuonesha upatanisho wa kisarufi. Makala yamehitimisha kwa kueleza dhana ya unyambulishaji, kuwa ni mchakato unaohusu kupachika mofu baada ya mzizi wa neno. Dhima kuu ya unyambulishaji katika Kiswahili huwa ni kuonesha matokeo ya tendo na kuzalisha kauli mbalimbali. Aidha, imebainishwa pia kuwa katika mazingira fulani unyambulishaji huweza kubadili kategoria ya neno kutoka kategoria moja ya neno kwenda kategoria nyingine. Ni imani yetu kuwa utata uliokuwa katika sarufi ya Kiswahili kwa miongo kadhaa kuhusu dhana za unyambulishaji na uambishaji, sasa umepata mwelekeo mpya.

**Marejeo**


Anderson, S. (1982). "Where's Morphology?" *Linguistic Inquiry* 13, 571-612.

Anderson, S. (1992). *A-morphous Morphology.* Cambridge University Press, Cambridge.

Aronoff, M. (1994). *Morphology by Itself*. MA: MIT Press.

Khamis, A. M. (2009). *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Sarufi* 1. Dar es Salaam:.Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Kihore, Y. M na wenzake. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

Kihore, Y. M. (2009). *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Sarufi 2.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili,.

Nkwera, V. F. (1978). *Sarufi Fasihi Uandishi wa Vitabu: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Creative Prints Ltd,

Nyangwine, N. na J. A. Masebo. (2007). *Nadharia ya Lugha ya Kiswahili 1: Kidato cha 5 & 6*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers,

Rubanza, Y. I. (1996). *Mofolojia ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TUKI. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.